

Mpendwa Rafiki,

Ni matumaini yetu kwamba barua hii itakukuta ukiwa katika afya njema.

Tunajua jinsi gani kuna umuhimu wa kupeana moyo wenyewe kwa wenyewe katika ahadi yetu ya kutokomeza umaskini uliokithiri katika dunia ya leo. Mwanzo wa barua hii, tungependa kuwapa habari na kusoma ushuhuda wenu na wetu. Inathibitishwa na ahadi ya kila mtu katika umuhimu wa kupambana na umaskini uliokithiri.

Ushuhuda wa kwanza ni kuhusu wamama wawili wanaosaidia kuendeleza huduma ya upatikanaji wa vitabu vya watoto katika kitongoji chao.

Dear Friend,

We hope this letter finds you in good health.

We know how important it is to encourage each other in our commitments to eradicate extreme poverty in today's world. Starting with this letter, we would like to give a place to tell and to read yours and our testimonies. It is to demonstrate everybody's commitment in the fight against poverty is important.

The first testimony is about two mothers helping to improve children's access to books in their neighborhood.

Kila wiki kwa muda wa miaka mitano sasa wanachama wa timu ya ATD wanakwenda Uwanja wa Fisi, moja ya vitongoji katika jiji la Dar es Salaam. Wanapeleka vitabu na wanawasomea hadithi watoto kama sabini hivi, kuanzia umri wa miaka 2 hadi 12. Wazazi wanafuraha kwa sababu watoto wao wanajifunza kupenda vitabu. Wazazi wanajua umuhimu gani kwa watoto wao kwa wakati ujao. Kidogo kidogo uamiminifu uliundwa kati ya wazazi na wanachama wa timu ya ATD.

Every week, for 5 years now, ATD team members go to Uwanja wa Fisi, a neighborhood in Dar-es-Salaam. They bring some books and read stories to about seventy children, from 2 to 12 years old. The parents are happy because their children learn to love books. Parents know what is important for the future of their children. Little by little, trust was created between the parents and the team members.





Miezi 2 iliyopita, Mama S na Mama W walianza kujihusisha zaidi kila wiki katika hii maktaba ya mtaa. Mwanzoni Mama S alikuwa anasaidia kuwapa watoto karatasi na pencil pale ilipofikia hatua ya watoto kuchora. Siku moja Mama S alipendekeza kuwasoma hadithi kwa watoto yeye mwenye.

Mama W kwanza aliuliza kama angeweza kuazima baadhi ya vitabu kusoma nyumbani yeye mwenyewe na kwa watoto wake. Lakini sasa huyu Mama siku zote anatoa msaada kwa Issa na Peter, kuzunguka katika kitongoji hicho kuwaazimisha na kukusanya vitabu kwa familia nyengine.

Ni kitu chenye manufaa sana kupata msaada wa hawa wamama wawili. Wana wafahamu watoto vizuri na wanachangia kuunda ari ya heshima na amani. Kuwepo kwao kunaruhusu makundi mawili katika maktaba ya mtaa, kutokana na umri walionao watoto: Mama S au Mama W huwasomea hadithi watoto wenye umri mdogo, wakati wanachama wa timu ya ATD huwasomea hadithi na kuijadili na watoto ambao tayari wameshaanza shule.

Mfano huu unaonyesha kwamba kila mtu anaweza kufanya, vizuri mahali alipo, katika kuleta mabadiliko ya maisha ya kila siku na kwa siku zijazo; kama wanavyo fanya Mama S na Mama W.

Two months ago, Mama S and Mama W started to be more involved every week in this street library. At the beginning, Mama S was helping to give out paper and pencils to the children when it came to drawing time. Then, one day, she proposed to read a story to the children herself.

Mama W first asked if she could borrow some books to read at home herself and to her children. Now, she helps Issa and Peter to regularly lend books to other families, to collect them back, and to circulate the books in the neighborhood.

It's very useful to have the help of these two mothers. They know the children well and contribute to create a spirit of respect and peace. Their presence allows two groups in the street library according to the age of the children : Mama S or Mama W read a story to the smaller children, while ATD team members read a story and discuss it with the children that already go to school.

This example shows that everybody is able to act, right where they are, by making a change in daily life and thus in the future; like Mama S and Mama W.

Habari nyingine...

Wiki chache zilizopita mwezi wa Machi, ATD ilikusanya marafiki zake katika Dar es Salaam kwa sababu ya mkutano. Katika hao marafiki wengi wao walitokea Dar es Salaam, lakini baadhi yao walitokea Dodoma, Moshi na Njombe. Pia washiriki katika mkutano walikuwa: Eugen Brand na Diana Skelton, wawakilishi wakuu wa mwenendo wetu wa kimataifa. Na Niek Tweehuysen, mtu wa kwanza wa ATD kujitolea katika Tanzania: walikuja kutoka Ufaransa rasmi kwa ajili ya mkutano.

Wakisababishwa na matukio mawili.



1. Nakala ya kwanza ya mkanda wa video kuhusu watu waliojiwekea ahadi ya kupambana na umaskini katika maisha yao ya kila siku katika Tanzania, ilitambulishwa. Kila mshiriki alishiriki kupeana uzoefu katika kujiwekea kwetu ahadi ndani ya jamii ya Watanzania. Maoni ya kila aliyehudhulia yalishawishi juu ya nini kiachwe kwa ajili ya nakala ya mwisho ya video.(je kitu gani kingemalizwa kwa ajili ya Octoba 17 mwaka huu)

And some news...

A few weeks ago, in March, ATD gathered some of its friends for a meeting in Dar-es-Salaam. The friends came mostly from Dar-es-Salaam, but some also came from Moshi, Njombe and Dodoma. Also participating in the meeting were: Eugen Brand and Diana Skelton, General delegates of our International Movement, and Niek Tweehuysen, first ATD volunteer in Tanzania: they came especially from France.

It was the occasion for two events :

1. The first version of a video about people in Tanzania that are committed in their daily life to fight poverty was presented. We shared our experiences and our different commitments within the Tanzanian society. Every participant's opinion was solicited on what is important to keep for the final version of the film (which should be completed by October 17th this year).

2. Saasita Constantine Munema, ni rafiki wa ATD kwa muda mrefu alitambulisha kijitabu "Maisha yake, Maisha yetu" ambacho amekitafsiri kwa Kiswahili. Kijitabu(*) kinahusu mahojiano ya Padre Joseph, muasisi wa mwendo wa ATD Dunia ya Nne. Kijitabu cha kwanza kuchapishwa katika Kiswahili kwa ATD.



2. Saasita Constantine Munema, friend of ATD for a long time, presented the booklet "His life, Our lives", that he translated into Swahili. The booklet(*) gathers interviews of Father Joseph, founder of the ATD Fourth World Movement. It is the first book published in Swahili by ATD.

Kijitabu na filamu vyote ni rahisi kuvitumia kama vitendea kazi (zana) kuvitambua na kuwasaidia wengine watambue mawazo ya mwendo wetu. Kama ungependa maelezo zaidi tafadhali usisite kuwasiliana nasi.

Both the film and the booklet are easy to use tools to discover and help others discover the ideas of our movement. If you would like more information, please do not hesitate to contact us.

(*) kuanzia sasa kijitabu kinapatikana na unaweza ukaagiza nakala kwa Tsh 500/= tu.

(*) The booklet is available as from now and you can order a copy for 500 Tsh.

Kila siku tunashuhudia kwamba watu wamejifunga kabisa wenyewe kufanya mambo kwa ajili ya wengine, walio maskini zaidi yao, wanafanya vitendo vya mshikamano na wengine, na wanapambana dhidi ya upweke wa umaskini uliopita kiasi. Tunasubiri wewe utuambie vitu gani unavyoviona au kuishi katika hisia hii. Tunaweza tukapeana hadithi hizi katika barua hii. Kumbuka, ahadi ya kila mtu ni muhimu ... na inatupa sisi uwezo.

Timu ya ATD Dunia ya Nne, Dar es Salaam

Everyday we witness that people commit themselves for others, poorer than them, act in solidarity with others, and fight against the isolation of the poorest. We wait for you to tell us what you observe or live in this sense. We can then share these stories in this letter. Remember, everybody's commitment is important... and gives us strength.

The ATD Fourth World team in Dar es Salaam



ATD Fourth World Movement
P.O. Box 61786
Dar es Salaam
mail : atd.tanzania@gmail.com
tel : 022 - 276 17 17